# *Nahed Chapman New American Academy*

1547 S. Theresa Avenue
St. Louis, MO 63104
Office 314-776-3285

slps.org/ncnaa
Saa: 8:05am - 3:02pm
Darasa: K-5

# DAFTARI LA

# MZAZI/MWANAFUNZI



***Twaamini Viongozi huubadili ulimwengu!***

*Nguvu kwetu huapatikana katika tofauti zetu!*

**SWAHILI**

## Kwa nini Duma ndicho kinyago chetu?

MwanziLISHIi wetu, Ms Nahed Chapman, alikuwa mtetezi mashuhuri, kwa shauku aliwapigania watoto waliokuja kwetu toka inchi tofauti duniani. Ingawa alikuwa mpole na mkarimu katika mbinu zake, alikuwa pia mwenye bidii kwa kuandaa njia ya kufunza Wanafunzi wa Lugha ya Kingereza kwa wahamiaji katika Shule za Umma za St. Louis. Hata kama Duma ina nguvu na uwezo, hawangurumi au kupaza juu sauti zao.

## MISSION

Twaamini Viongozi huubadili ulimwengu!

## MAONO

Tutakuwa vielelezo kwa Uongozi kwa ajili ya mafanikio ya huduma kwa mtoto wakati ujao.

## JUKUMU ZA DUMA

Viongozi huubadili ulimwengu!
Mimi ni Kiongozi!
Mimi ni mwaminifu.
Mimi ni mwenye Huruma.
Mimi ni mwenye Uthamini.
Mimi ninategemewa.
Mimi ni Kiongozi!
Mimi ninaubadili ulimwengu!

## MAWASILIANO

**Shule: 314-776-3285**
**Ofisi ya ESOL: 314-664-1066**

Tunawasiliana na familia kwa simu au ana kwa ana tukitumia mkalimani iwe ana kwa ana au kwa njia ya simu. Tunatuma pia ujumbe kwa simu uliorikodiwa kwa lugha mbali mbali ukiwa na taarifa maalum kwa familia zote.

Kiongozi wa shule, makamu wake, na mwalimu wa watoto wako watatuma ujumbe mfupi wakitumia pointi ya kuzungumza. Ujumbe utafika kwako kama ujumbe mfupi kwa simu. Unaweza pia kupakuwa programu, lakini siyo lazima. Wazazi wanaweza jibu au tuma ujumbe mfupi pia kwetu.

## MABADILIKO YA ANWANI NA NAMBA YA SIMU

**Ikiwa umebadili namba ya simu yako, tafadhali wasiliana na shule ili tujue na hivyo tuibadilishe katika mfumo wetu**. Tunataka kuwa na uhakika wa kuwasiliana nanyi kila mara. Ina umuhimu wake wakati mtoto wako amegonjwa au aumie shuleni na anahitaji kuchukuliwa nyumbani.

Ikiwa Anwani yako imebadilika, tafadhali ita shuleni utujulishe. Ushahidi (mkataba wa kukodi, mswada wa matumizi, k.z) italetwa kwetu ili tufanye mabadiliko katika mfumo wetu. Baada ya kubadili, twaweza omba usafiri wa mtoto upya.

## MWENENDO UNAOTARAJIWA

Wanafunzi Kwa Nahed Chapman New American Academy ni **Viongozi**!

Thamani ya Uongozi kwetu ni **Uaminifu, Huruma, Uthamini**, na **Kutegemewa**.

Tunaamini ni muhimu kufunza wanafunzi namna ya kudhihirisha Uaminifu, Huruma, Uthamini na Kutegemewa. Matriki yetu ya matarajio yapatikana kwa mwisho wa kitabu cha mwongozo.

Shule za Umma za St. Louis zimeandaa Kitabu cha Kanuni ya Mwenendo wa Mwanafunzi kwa kila mwanafunzi. Tafadhali someni kitabu hicho pamoja na watoto wako nyumbani. Wakati kutakuwa tatizo la mwenendo, taratibu za nidhamu katika kitabu cha Kanuni za Mwenendo zitatekelezwa.

## UHUDHURIAJI

Kusudi mtoto wako afanikiwe shuleni, ni lazima ahudhurie masomo kila siku tena kwa wakati. Wanafunzi wasipofika au wachelewe, ni vigumu kwao kujua maelezo au kufuata taratibu wakifika shuleni.

Ikiwa mtoto wako hatafika shuleni, tafadhali wasiliana na shule. Hivyo kutokufika kwake kutakuwa kumefahamika. Hata hivyo kukosa kufika ka mtoto wako kutahesabiwa zidi yake.

**Kuhudhuria shuleni ni shurti kwa jimbo la Missouri.** Wazazi wataitwa kwa simu, watapokea barua, na kutembelewa nyumbani na wafanyakazi ikiwa watoto wao hawafiki mara kwa mara. Ikiwa mwanafunzi amekosa siku 10 au zaidi, ripoti itatolewa kwa Idara ya Missouri ya Huduma za Watoto.

## CHAKULA CHA ASUBUI

Asubui na saa moja na dakika arobaini hadi saa mbili **(7:40 am-8:00 am**), kuna chakula bila malipo kwa wanafunzi wote.

## KUFIKA/KUONDOKA KILA SIKU

Kawaida shule huanza saa mbili na dakika tano (8:05am). Kuondoka kwa wanafunzi ni saa tisa na dakika mbili (3:02am).

Milango imefungwa kila siku. Hii kwa ajili ya usalama wa wanafunzi na wafanyakazi.

**Unapotembelea shule nenda kwa mlango 1 ulio mbele na bonyeza kwenye njunga. Unaporuhusiwa kuingia, tafadhali elekea kwa ofisi ya Uongozi.**

Usiwalete watoto wako shuleni **mbele** ya saa moja na thelathini na tano asubui (**7:35**). Ikiwa wanafunzi wanafika mbele ya saa mbili (8:00) lazima watumie mlango wa 2 upande wa mbele. Wafikapo nyuma ya saa mbili, watatumia mlango 1 na kubonyeza kwenye njunga.

**Mtoto hatachukuliwa na awaye yote ila wazazi, walezi halali, au wale walio na ruhusa ya kuchukua mtoto wako. Mzazi/mlezi lazima atoe nakala ya ruhusu kwa mtu mwengine kuweza kuchukua mtoto wao shuleni.**

## KUONDOKA MAPEMA

Tafadhali mchukuwe mtoto wako mapema ikiwa ni dharura au miadi ya lazima. Kuondoka mapema ni changamoto kwa taratibu za majifunzo si kwa mtoto wako pekee, bali kwa watoto wote darasani. Kuondoka mapema itachukuliwa na kuhesabiwa kuwa kosa la uhudhuriaji kwa mtoto wako.

Ukihitaji kumchukuwa mtoto wako mapema, tafadhali ita au tuma ujumbe shuleni mbele ya wakati. Watoto siyo lazima wachukuliwe kati ya saa nane na nus na saa tisa (2:30 na 3:00). Hii inaingilia kati taratibu zetu za kuondoka.

## UCHUKUZI WA MTOTO NA SAA TISA 3:00

Ukihitaji kumchukuwa mtoto wako saa za kuondoka shuleni, mzazi au mlezi unapashwa kuita au kutuma ujumbe shuleni mbele ya saa nane 2:00 ili kutujulisha.

Ukija kumchukuwa mtoto wako, ongoza gari lako hadi mwisho wa Theresa Ave na ubaki ndani. Tutamtoa nje mtoto wako kwa mlango wa mbele wa shule na saa tisa 3:00.

## SIMU ZA MKONONI

Wanafunzi hawastahili kuwa na simu za mkononi shuleni. Mwanafunzi atakapoonekana na simu, ataarifiwa mara moja kuiweka kando. Asipotii na ionekane tena, itachukuliwa na kuchungwa na kiongozi au makamu wa kiongozi. Mzazi/mlezi ndiye atayeichukuwa. ***Shule halihusiki na kupotea au kuibwa kwa simu za mkononi.***

## MAVAZI YAFAAYO SHULENI

Ni **Shurti** kuvaa sare za shule kwa Nahed Chapman New American Academy.
Sare za shule ni zifuatazo:

- Shati ya polo yenye kola ambayo ni rangi ya samawati hafifu, Nili, Nyekundu, au Nyeupe yenye vifungo viwili
- Suruali ndefu ya rangi ya majani makavu au Nili
- Kaptula ya rangi ya majani makavu au Nili au sketi ya urefu unaofaa

Wanafunzi hawaruhusiwi kuvaa yafuatayo:

- Mavazi yanayoonyesha mwili kupita kiasi kama vile: sketi fupi, kaptula fupi, marinda mafupi/yanayobana, blauzi zenye mikanda inayofanana na tambi, blauzi zinazoonyesha mwili kupita kiasi
- Blauzi zinazoonyesha tumbo/kitofu na/au kifua; suruali zenye matundu; suruali zinazoshuka chini kiunoni na kuonyesha kaptula ya ndani, chupi au matako
- Mavazi yanayotangaza pombe, tumbako, au madawa ya kulevya, mavazi yenye maandishi machafu, yanayoelekea ngono, ishara za magenge na kadhalika
- Mavazi mengine yoyote yanayobainiwa na Kiongozi wa shule kuwa si mazuri kwa kawaida ya shule.

Mapashwa mengine:

- Kofia za aina yoyote haziruhusiwi kuvaliwa ndani ya jengo la shule.
- Nguo zote za sketi lazima zitambuke cha za vidole vya mikono inyoshwapo kwenda chini kwenye miguu.
- Blauzi au shati lazima ziingizwe ndani ya suruali.
- Viatu lazima viwe vya kufunga vizuri miguuni (hakuna kandambili au vyenye kuteleza)

## HALI MBAYA YA HEWA

Vituo vya redio na televisheni za mahali zitaripoti kwamba shule zitafungwa kama iliamuriwa na Msimamizi wa shule. Kufungwa kwa shule pia itaripotiwa kwenye tofuti ya wilaya (www.slps.org).

Shule likiwa limefungwa, hakuna mfanyakazi yeyote kwa Nahed Chapman New American Academy.

## KANUNI/SHERIA ZA BASI

Shule za Umma za St. Louis zina mikataba na Missouri Central School Bus kwa mabasi yake. Wazazi waweza kupakuwa "Here Comes the Bus" ili kufuata basi inavyokuja. Uongozi wa namna ya kupakuwa hiyo programu ni tayari katika lugha tofauti. Unaweza pata uongozi huo kwa linki hapa chini. Utahitaji namba ya mwanafunzi wako kwa kutimiza taratibu. https://www.slps.org/Page/76310

Wanafunzi wote lazima kufuata kanuni zilizowekwa na Sera ya Bodi ya Shule za SLPS wanapotumia mabasi kwelekea na kutoka shuleni. Wazazi na wanafunzi lazima wakumbuke, kupewa basi ni marupurupu, siyo haki, inamaanisha itaondolewa kama mwenendo wa wanafunzi hauridhishi.

Usalama ni muhimu kwa usafirishaji wa wanafunzi kwa kwenda na kutoka shuleni. Dereva lazima awe makini kwa kutembeza basi na asivutwe mawazo na mwenendo wa mwanafunzi.

Mwanafunzi akihatarisha usalama wa wengine wakiwa ndani ya basi, dereva atajaza ripoti ya nidhamu na kuituma kwa Kiongozi au makamu wake. Kufuatana na ukiukaji wa kanuni, wanafunzi wameza kuondolewa utumizi wa basi kwa muda kama ilivyo amuriwa. Wanafunzi wakipoteza utumizi wa basi kwa muda, wataendelea kufika shuleni. Wazazi ndio watahusika na usafiri wa wanafunzi kwenda na kutoka shuleni wanapo simamishwa kutumia basi kwa muda.

Mzazi/mlezi lazima awe kwenye kituo cha basi kwa kungoja wanafunzi wa darasa la chekechea na la kwanza watokapo shuleni. Ikiwa mwanafunzi wa chekechea au wa darasa la kwanza atatoka kwenye basi na kuenda na ndugu yake mkubwa, lazima awe amepewa ruhusa iliyoandikwa na mzazi/mlezi.

## VYOMBO KUPOTEA/KUIBWA

Hesabu kubwa ya pesa, vyombo vya kucheza, michezo, na/au simu za mkononi haviruhusiwi kuletwa shuleni.

Shule halihusiki na uwekaji wa vitu vyovyote, pesa, au vyombo binafsi vya mtu vilivyo chungwa vibaya au kuibwa.

Shule halitahusika katika lolote ili kutafuta kitu binafsi kilichopotea au kuibwa.

## DAWA KWA WANAFUNZI

Ikiwezekana, dawa lazima zichukuliwe nyumbani.

Ikiwa dawa itatolewa shuleni na muuguzi wa shule, lazima dawa hizo ziletwe zikiwa na yafuatayo:

- ✓ Barua toka kwa mganga kujulisha dawa itachukuliwa shuleni
- ✓ Barua ya ruhusa toka kwa mzazi (iwekwe kwa muuguzi wa shule)
- ✓ Dawa zote **lazima** ziwe katika kontena yake tangu farmasia/duka la dawa.
  Jina la Mganga na anwani ya farmasia

Dawa zikitumwa shuleni bila barua ya mganga haziruhusiwi kuchukuliwa shuleni.

Wazazi wanaruhusiwa na wanahimizwa kupana dawa kwa mwanafuzi shuleni, wakati wote iwezekanavyo.

## WATOTO WAGONJWA

Mtoto wako akigonjwa tangu shuleni, muuguzi atawasiliana nawe ili uje kumchukuwa.

Mzazi, mlezi, au mtu aliye muasiliani wa dharura, na kuorodheshwa kwenye fomu ya rufaa ya dharura lazima aje kuchukuwa mtoto mara tu anapoitwa.

Mtoto wako hatachukuliwa na mtu asiyekuwa kwa orodha iliyo kwa fomu ya rufaa ya dharura.

**Uhakikishe kwamba una simu namba ya kazi wakati wote kwenye faili ofisini.**

## MIKUTANO YA WAZAZI

Mikutano ya wazazi itafanyika mara pili mwakani, mwezi Oktoba na Machi. Ni shurti kwako kuhudhuria mikutano hiyo.

Wazazi wazeza kuratibu mikutano wakati mwingine mwakani. Tafadhali wasiliana na mwalimu wa mtoto wako au Kiongozi wa shule il kuratibu mkutano. Tafadhali usijitokeze tu na kufikiri kwamba utasema na mwalimu wa mtoto wako. Walimu kila siku wanahusika zaidi na wanafunzi wao, kufunza masomo. Walimu waweza kujiweka tayari kufuatana na walivyopanga muda wao ili mkutane.

## KUJITOLEA

Wazazi, viongozi wa jamii, rafiki na ndugu wanaalikwa kujitolea kwa Nahed Chapman New American Academy.

Ikiwa unahitaji kusaidia kwa hiyari, tafadhali tembelea shule utapewa karatasi za kujaza au wasiliana na mtaalamu wa jamii na famiia kupewa taarifa zaidi.

| *Shule la NCNAA-orodha ya maadili tofauti.* | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Darasani** | **Ukumbi** | **Choo** | **Mkahawa** | **Basi** | **Kuwasili/Kuondoka** | **Uwanja wa michezo** |
| **Kiwango cha sauti** | Inategemea | 1 | 0 | 2 | 1 | 1 | Inategemea |
| **Uaminifu (Pekee, Wengine, Mali)** | Chunga mikono, miguu na vyombo vyako.<br><br>Uwe mwaminifu kwako mwenyewe na kwa wengine. | Kuelekea haki. | Ingia/toka kwa wakati ufaao.<br><br>Chunga maji ndani ya sinki tu.<br><br>Tunza vizuri raslimali za choo.<br><br>Safisha baada ya matumizi binafsi na ya wengine. | Chagua kwa haraka chakula chako.<br><br>Baki kwenye mstari.<br><br>Safisha baada ya matumizi binafsi na ya wengine. | Msikiliza dereva kwa makini.<br><br>Keti ukitazama mbele.<br><br>Weka mikono na vitu vingine ndani ya basi.<br><br>Baki ukiketi wakati wote wa safari.<br><br>Shika vitu vyako kwenye mapaji. | Panda na Ushuke basi kwa utaratibu.<br><br>Tazama ngambo zote kabla uvuke barabara.<br><br>Uingiapo ndani ya basi kaa mara moja. | Tumia vifaa ipasavyo.<br><br>Amua kwa usalama wako. |
| **Huruma** | Sikiliza wengine wasemapo na usubiri zamu yako | Tabasamu na upunge mkono kwa wapitao mbele yako | Ikiwa mtu anahitaji msaada, ambia mtu mzima. | Keti na rafiki mbali mbali.<br><br>Waite wanaoketi pekee waje mkae pamoja. | Tazama wanafunzi wanaohitaji msaada na uwasaidie. | Kwa kutoka ndani ya basi subiri zamu yako.<br><br>Waache watoto wadogo waingie na watoke kwanza. | Kubali wewe na wengine kutenda kosa.<br><br>Wahusishe wengine. |
| **Kuthamini** | Tumia usemi mzuri na ifaavyo | Tembea kwa utulivu.<br><br>Weka mikono yako karibu na mwili wako.<br><br>Usishike ubao ulio karibu na ukumbi ukitembea. | Usiwaangalie wengine.<br><br>Okota taka na uzitupe kwenye pipa la taka.<br><br>Vuta maji baada ya kutumia choo.<br>Tembea kwa makini<br><br>Funga maji. | Fuata uongozi wa wafanyakazi mara tu unapotolewa.<br><br>Tumia usemi mzuri.<br>Sema tafadhali na aksante. | Panda basi kwa utaratibu ufaao.<br><br>Tumia usemi mzuri na ifaavyo.<br><br>Sikiliza dereva kwa makini.<br><br>Okota taka na uitupe kwenye pipa ya taka. | Tumia usemi mzuri na ifaavyo.<br><br>Ondoa kofia kichwani unapokuwa ndani ya jengo la shule. | Shiriki.<br><br>Kwa uvumilivu subiri zamu yako.<br><br>Jipe moyo ushindwapo kwenye mchezo. |
| **Kutegemewa** | Fanya uwezavyo.<br><br>Fuata maelekezo mara tu yanapotolewa. | Nenda mara moja darasani.<br><br>Omba ruhusa wakati wowote.<br><br>Okota taka na uzitupe kwenye pipa. | Ripoti visa vya maandishi ukutani au hasara kwa wafanyakazi.<br><br>Tupa taulo za karatasi kwenye pipa la taka. | Wakuombapo, safisha nafasi yako na tupa uchafu kwenye pipa.<br><br>Ujue namba yako kwa akili. | Tumia basi yako tu.<br><br>Hakikisha kaka na dada zako wako kwenye basi. | Tulia na ungoje maagizo kwenye msatari.<br><br>Fika dakika 10 mapema kwenye kituo cha basi.<br><br>Vaa sare yako ya shule.<br><br>Fika shuleni ukiwa tayari na vifaa vyako vyote. | Tunza vifaa vyako. |